
Kumpata Mungu!

Wapi? Na Vipi?



Gabriele

Kumpata Mungu!

Wapi? Na Vipi?

Maandishi ya Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu
kwa wakati wetu



First Edition in Swahili: October 2021
1ère édition en Swahili: Octobre 2021

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:
Gott finden! Wo? Wie?

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Kumpata Mungu! *Wapi? Na Vipi?*

Wakati wetu ni wa wasiwasi na misukosuko. Watu wengi zaidi hujiswali maswali juu ya Mungu:
Je, Mungu yupo wapi?
Twaweza kumpata vipi?
Au Kweli Mungu yupo?
Ikiwa Mungu yupo, kwa nini hajitokezi?

Au tena: *Siamini Mungu kwakuwa, ukichunguza kwa makini matukio ya ulimwengu huu, utatambua hakika kwamba hakuna Mungu.*

Mtu mwengine atasema: *Wakati tunapotaka kujua kwa nini Mungu anavumilia machafuko kama hayo katika ulimwengu wetu, baadhi ya dini husema ni siri ya Mungu.*

Akitafakari sana, atasema:
Nilitafuta katika dini tofauti na nilidhani hapa au pale, nimepata chembe ya ukweli. Wakati mwingine, baada ya kukubali chembe fulani za ukweli, nikaamini kwamba nimefikia lengo, na mwishowe nikawa mwanamemba wa dini hiyo. Lakini, haraka sana, mashaka yakanitawala na maswali yakaibuka: Chembe hiyo ya ukweli ina mafaa gani, kwani haijanibadilisha bado, hata kama nimeahidiwa hivyo. Kama mtu asiye na uaminifu na mwenye wasiwasi, nikahakikisha kwamba kuna dini nyingine zilizo na ukweli wa milele. Je, tukikusanya chembe za ukweli za dini tofauti, Tutaweza kumpata Mungu?

Kukata tamaa kwangu kukazidi kuongezeka na nikasema haya: Nilitafuta na kutafuta mara tena, sikuona wala kumpata Mungu baada ya kuingia katika dini nyingi.

Tafakari hizi zimenituma kufikiria kwamba, hakika, si mimi tu ndiye najiswali swali hili: Mungu yuko wapi? Tutampata wapi?
Kwa nini hujificha kwetu wakati tunapokubali ukweli tunaoambiwa kuhusu yeye?

Licha ya hayo, sitaacha utafiti wangu, ingawaje mashaka yangu kuhusu uwepo wa Mungu yanaongezeka siku baada ya siku, hasa zaidi ninapoona mavazi ya viongozi wa kidini wanaomwakilisha kwa nje.

Ninajiswali kwanini Mungu hukubali mwonekano bandia wa wanaojiita wakilishi wake na sifa nyingi juu yao? Na wakivaa mavazi ya gharama kubwa, wanahubiri unyenyekevu, ijapokuwa watu wengi wana njaa, hawana makao na uwezo wa kuvaa vizuri. Nikaanza mara tena kuwa na mashaka juu ya kuwepo

kwa Mungu. Taji zao zilizopambwa kwa mawe ya thamani, hata pia kofia zao zinazofunika upaa wao, huibua maswali ndani mwangu.

Kwa nini haya yote huhitajika?
Je tunajiswali hakika kile kinachojificha nyuma ya hayo?
Katika mazungumzo na wamoja kati ya wakilishi wa Mungu, tunafikia kutambua kwamba wapo mbali zaidi na ukweli kuliko mtafiti mpya wa Mungu aliye na imani.

Mtafiti wa Mungu amegundua kwamba:
Viongozi wote wa kidini husadiki kwamba dini yao ndiyo inayoleta wokovu, na kwamba ndiyo tu iliyo na ukweli.



Wasomaji wapendwa, mkitaka, fikirieni juu ya jambo lifuatalo:
Hakuna haja ya kwenda hapa na pale kwa kumpata Mungu. Kwanini? Kwa sababu, Roho wa milele, anayeitwa Mungu katika nchi za magharibi, yupo mahali pote, na kwa hivyo pia yupo katika nafsi ya kila mwanadamu.
Roho huru asiye na mwisho, Roho aliye popote, Mungu, hupatikana katika viumbe vyote, katika kila mti, katika kila mmea mdogo, kwenye majani, katika mnyama na katika jiwe. Ndani ya ulimwengu wenye nguvu mnapatikana Roho wa milele anayefanya kazi ndani ya vitu vyote.
Kwa kumpata Mungu, hatuna haja ya kwenda hapa na pale.
Kwa kuomba Mungu, hatuna haja ya kujificha. Hebu tufikirie juu ya maneno haya ya Yesu wa Nazareti: (Matayo 6:28) *"Angalieni jinsi maua ya shamba yanavyokomaa, hayatendi kazi wala*

kufuma lakini, ninawambieni kwamba hata Suleimani katika utukufu wake wote, hakuvaa mavazi kama mmoja wao."
Kwa hiyo Mungu yumo ndani mwetu. Mungu yupo karibu nasi. Mungu yupo juu na chini yetu, kuume na kushoto kwetu. Yeye ni Roho huru, Uzima ndani ya vitu vyote.

Hata kama tunamtafuta Mungu kwa bidii katika dini, katika mashirika au vikundi vya kiroho, hata kama tuna dhamiri, na vichocheo ndani ya makanisa ya kishirika, baada ya muda, vyote huwa bure na bila mafaa. Kwani mtu ambaye hakumpata Mungu ndani ya nafsi yake, huendelea kumtafuta toka dini moja hadi nyingine, toka shirika au kikundi kimoja cha kiroho hadi kingine.

Kwa kumkaribia Yeye, Mungu, Wamilele, ametutolea Amri kumi, kupitia Musa na kupitia Yesu wa Nazareti, ametutolea

mafundisho ya mbinguni inayopatikana katika Mafundisho yake mlimani. Amri kuni na mafundisho ya Yesu wa Nazareti ni dondoo tu za Sheria ya milele, ya ulimwenguni pote ya Mungu, ya upendo na uhuru wake, ambavyo ni uzima halisi.

Kwa upande mwingine, mtu anayeupatia thamani kubwa mwonekano wake wa nje kuliko Mungu, na anayetosheka tu na kuwa na imani na anayefuata mila na desturi za dini za nje, hatampata kamwe Mungu, hata kama anafikiria kwamba amepata hapa na pale ukweli.

Siku moja au nyingine, cheche hizo za ukweli hufifia. Mwanadamu ataendelea kumtafuta Mungu na kuendelea kutoridhika, hadi muda ambapo mwanadamu na nafsi watakapopata ndani mwao asili yao, chimbuko la Uzima na hadi nafsi itakapobaki ndani ya bahari ya Uzima.

Hasa kwa sasa, watu wengi hujiswali kwa nini Mungu alitutolea Amri kumi na kwa nini Yesu wa Nazareti alitutolea mafundisho yake ya mlimani?
Je, ujuzi wa Amri kumi za Mungu na mafundisho ya Yesu mlimani umetufanya wenyi akili sana, na kutuweka karibu na Mungu?

Kama tulivyosema hivi karibuni, kwa kumpata Mungu, hakuna haja ya dini ya nje au mpatanishi, wala haja ya mashirika inayowashikilia wanamemba wao na iliyo na wapatanishi.

Ni sisi, peke yetu, ndiyo tungelipashwa kumtafuta Mungu na kumpata ndani ya nafsi yetu, kwa sababu Yesu wa Nazareti alitufundisha kwamba Mungu yumo ndani mwetu na alituonyesha jinsi inatupasa kuomba akisema:
“Lakini wewe, unapoomba, ingia kwenye chumba kilicho ndani sana, funga mlango

na umuombe Baba yako aliye katika siri; na Baba yako aonaye katika siri atakujibu."

Yule anayeamini mafundisho ya Yesu wa Nazareti, anaamini bila shaka uwepo wa nafsi isiyokufa, ambamo anakaa na kutenda Roho huru na wa milele, wa asiye na mwisho ambaye watu wa magharibi humuita Mungu.

Sisi wanadamu, tuna tabia ya kulaumu wengine kwa chochote kibaya kinachotupata. Tunanyooshea kidole kile ambacho wengine wanafanya au wasichokifanya. Daima tunawapa watu wengine wajibu wa kosa la kutenda vibaya au la kutofanya kile ambacho wangelipashwa kufanya. Inatupasa kubadili mtazamo wetu wa mambo na kuelewa kwamba kila mmoja wetu ana wajibu wa maisha yake mwenyewe hapa duniani, na wa kile anachokifanya na

asichokifanya. Ni vema sisi wenyewe tutambue jambo mbaya katika hisi, hisia, mawazo, maneno na matendo yetu.

Mtu anayejitahidi kujichunguza sana, atagundua kuwa yeye ni kama mnafiki kwani hisi, fikra, maneno na matendo yake, ni kila mara tofauti sana na mwonekano wake au pia kile anachowafanya watu wengine waamini.

Tupo kama wanafiki. Mwishowe tunatenda dhidi yetu wenyewe, dhidi ya nuru ya nafsi yetu, na tena dhidi ya mwili wetu unaoteswa na hata kuugua kwa sababu ya umbali wake na Mungu.

Tunajitendea wenyewe kile tusichokitaka. Wajibikaji wa kile kinachotupata si wengine. Sisi ndiyo wakosaji!

Kosa letu hujificha nyuma ya mwenendo, hisia, mawazo, maneno na matendo yetu.

Hivyo ndivyo tulivyo na ndivyo tunafanya uovu.

Siku moja au nyingine, tutatambua makosa yetu, na kwa unyenyekevu, tutamuomba msaada na uungaji mkono Roho aliye popote.
Inatupasa kumuendea Mungu, kufanya hatua ya kwanza tukielekea kwake kwa kushinda uovu wetu kwa msaada wake. Yule anayechunguza hali zake mbovu akizingatia Amri kumi na mafundisho ya Yesu wa Nazareti, hutambua upesi kuwa amejitenga na Mungu.
Wasiwasi, dhiki, mateso au ugonjwa vingelitusaidia kutafakari juu ya jambo tulilosababisha wenyewe badala ya kumtaja Mungu kama mwajibikaji wa shida zetu. Dalili zote hizo, pamoja na kutoridhika kwetu, vinaonyesha kwamba tunamtafuta Mungu.

Tukubali au la, kila mmoja wetu hajaridhika bado, kwa sababu nafsi yetu inamtafuta Mungu, nchi yetu ya milele, bahari ya uzima halisi, kwani kiumbe safi cha nafsini mwetu, ambacho ni sisi, kina asili yake katika uwepo safi wa milele.

Wasomaji wapendwa, yule anayetafakari mara na mara juu yake mwenyewe, anaweza kuhisi kutoridhika kwake na kwamba kwa kweli anatafuta lengo la milele. Hata kama hatutaki kuyakubali, siku moja au nyingine, tutahisi uchungu fulani moyoni mwetu. Ni kumbukumbu ya asili yetu, nia kubwa ya kurudi nyumbani, kwa Baba wa milele, katika ufalme wa Mungu, katika nchi yetu ya milele.

Wakati wa ujana, kuna vitu vingi tusivyotaka kuona. Tunadhani kupata raha ya kudumu na kutosheka sana katika mambo inayotufurahisha na kutuvutia.

Hakika ni kudanganyika tu, kwa sababu katika ulimwengu wa muda, hakuna kitu kinachodumu. Kutokana na umri wao, watu wengi hutambua kwamba hawajaridhika bado na kwamba mara na mara walitafuta kitu fulani, bila kukijua, ijapokuwa ulimwengu huu umewapa sifa zote na mali walizohitaji.

Moja kwa moja au la, wanadamu wote na nafsi zote zinatafuta lengo la milele, mkondo wa milele, bahari ya uzima. Kila mmoja wetu angepashwa kutambua kwamba, yeye ni msafiri duniani ambaye, siku moja au nyingine ataacha vazi lake la kidunia na ni nini kinachotokea basi?

Hata kama watu wamoja wanalaghai jirani zao na kuishi duniani katika tamaa ya mali na ufisadi, kila mtu siku moja atajiswali: Je, haya yote yamenifalia nini? Nimefanyia nini nafsi yangu, itabeba nini itakapoaga dunia hii?

Yule anayesadiki uzima baada ya maisha ya dunia hii, analazimishwa kujiswali, ni wapi yeye au nafsi yake itakapoenda.

Aina yote ya kutoridhika hutuonyesha kwamba nafsi yetu ujidhihirisha ndani mwetu. Inabisha mlangoni mwa hisi, na dhamiri yetu, kwani imejitenga na njia yake iendayo kwenye maskani kwa Baba wa milele. Vilevile inabisha mlangoni mwa fikra, maneno na matendo ya mwanadamu.

Onyo hili litokalo ndani ya nafsi yetu, ni mwito wa kumrudilia Mungu na kuingia hekaluni mwa Mtakatifu mno, ndani ya nafsi yetu kwa ajili ya kufuata maelekezo ya Amri kumi na ya mafundisho ya Yesu wa Nazareti.

Njia iongozayo kwenyi asili ya nafsi yetu ni hatimaye kuweka mpango mzuri ndani ya moyo wetu. Yule asiyejiswali ili

ajue nini iliyo katika hisi, fikra matendo, na tabia yake yote, hufanana na meli iliyoacha njia baharini. Wakati mmoja au mwingine, meli hupinduka bila ya mabaharia wake kujua mahali meli ilipozamia. Hofu itatanda! Mmoja wa mabaharia ataomba msaada, mwengine atamlilia Mungu, wa tatu ataita timu la uokoaji.

Kila mmoja atategemea kujiokoa mwenyewe, au kuokoa mwili wake. Je, ni wanani watakaookolewa hima, kati ya wale wanaoomba msaada wa dunia hii na wale wanaomlilia Mungu kwa moyo wa dhati?
Kila mmoja ataweza kujibu swali hili mwenyewe na kuchagua mahali pa kuelekeza mwito wake.



Walimwengu huzungumzia kuhusu miujiza. Kwa mfano: “Huu ni muujiza!” Ila, maishani mwetu duniani, hakuna muujiza, kuna msaada kamili tu toka upendo na huduma unaojaa upendo wa Mungu. Sheria ya milele ya Mungu ni sheria ya upendo na ya huduma inayojaa upendo kwa kila kiumbe.
Ndani ya sheria ya Uzima unao jumuisha vyote na ulio umoja, hamna kupunga pepo wala uvumba, wala kujitesa wala kujisifu, wala pia sherehe, ibada ya mapadri, au ya sala zilizoandaliwa tayari. Hakuna misionari mchungaji, wala maabudu, ibada ya sadaka, dini ya nje, mabaki ya mifupa, wala mtakatifu, mnafiki wala maaabudu ya sanamu au kujiabudu. Sheria ya Mungu ni halali kwa watu wote, kwa “aliye kwenye meli inayovunjika”, hata awe amenusurika au amezama.

Yule anayejichukua kama muamini, anapashwa kujua mafundisho ya Yesu

wa Nazareth kuhusu mpango mzuri wa hekalu na kujua kwamba kila mwanadamu ni hekalu la Roho mtakatifu. Inampasa kukumbuka ujumbe huu wakati anapoomba hata pia wakati anapotaka kwenda hekaluni lililo jengwa na mikono ya wanadamu. Atagundua haraka kwamba amekuwa huru na mwenye dhamiri ya uwepo wa Mungu.

Yeyote anayechunga maneno ya Yesu dhamirini mwake hahitaji ubishi wote wa mapadri na wachungaji, bali tu mafundisho makuu yanayosema: Mungu ni Roho huru, Roho aliye pote anayeishi katika mazingira na ndani ya mnyama, na pia inayochochea uhai wa mawe, dunia nzima na ulimwengu wote.

Kila mwanadamu ni kama mtu anayezama na anayeteseka katika kisiwa anachokiita dunia. Nafsi yake itaenda wapi baada ya kufa kwake? Saa ya kufa

ikitimia, kila mwanadamu hutamani nafsi yake ifike kwenye bahari ya upendo wa milele na kuishi humo milele.
Ni mwaliko wa nafsi yetu inayotegemea ndani mwake nchi yake ya milele.

Wasomaji wapendwa, ikiwa mnaweza kuthibitisha uwepo wa Roho huru, bila ibada wala ubunifu uliofanywa kuhusu "Mungu", utapiga hatua kukaribia Amri kumi za Mungu na mafundisho ya Yesu wa Nazareti, pia mafundisho yake mlimani.



Sisi ni nani kwa kusema hayo?
Sisi ni warithi wa Yesu wa Nazareti aliyefundisha Roho huru, Mungu, na alionyesha kupitia mfano wa maisha yake kwamba, kwa kumkaribia Mungu, mwanadamu hana haja ya mashuruti, kanuni, au ibada, wala mapadri au wachungaji.

Warithi wa Yesu wa Nazareti hawaundi dini la nje wala shirika ya kidini, inayoongozwa na kiongozi wanayemfuata kama vipofu. Kinachowajumuisha warithi wa Yesu wa Nazareti ni kuhisi ukaribu wa kindugu na maelewano, kwa sababu wote ni wana wa Roho huru.

Yesu wa Nazareti aliwaambia watu karibu maneno haya: Mahali ambapo watu wawili au watatu wamejumuika kwa jina langu. Mimi niko kati yao. Mara kwa mara, watu hujiuliza, ni wapi wanapoweza kupata aina hii ya jamii huru.

Kituo cha kimataifa cha ukristu asilia kwa tamaduni zote, kinachotenda kazi ulimwenguni pote ya Kristo wa Mungu, kina jamii huru na yenye upendo inayoweza kumpa taarifa yule anayeitafuta kwa dhati. Kwa wale wote wanaotafuta jamii iliyo wazi na huru, tunatoa ushauri huu: ikiwa mnawafahamu watu ambao walio na matakwa kama na yenu, mnaweza kukusanyika mara kwa mara kwa kusali au kubadilishana ujuzi wenu wa kiroho, kwa lengo la kijifunza wamoja kwa wengine, kukua na kukomaa kiroho.

Mara nyingine: mwanadamu hana haja ya dini ya nje, mila na desturi za kidini. Kila mmoja wetu anapashwa kutafakari na kuwa na dhamiri kwamba Mungu yumo ndani ya kila mtu, ndani ya nafsi ya kila mtu. Warithi wa Yesu wa Nazareti huomba jinsi moyo wao unavyowaamuru, bila kutumia sala

zilizoandaliwa tayari, wakigeukia ndani mwao.

Ingawaje Mungu, Roho wa Baba wa mbinguni, anajua vitu vyote, wamoja wanahisi hitaji la kuzungumza naye. Huko ndiko kueleza kinachotugusa moyoni. Yule anayeomba, anaombea nafsini mwake, akijitoa kwa Mungu moyoni mwake. Maombi ya ndani na utekelezaji hatua kwa hatua wa Amri kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa, hata pia mafundisho ya Yesu wa Nazareti, hutusaidia kutambua dhambi zetu, kuzitubu, na kuzirekebisha na kutozitenda tena.

Sala ya moyoni na iliyo huru husababisha maendeleo na ukomavu wa kiroho na utajiri wa maisha halisi, wa uhuru, wa maelewano na zaidi utajiri wa upendo wa Mungu na wa jirani yetu. Njia hii ya kiroho, njia ya uhuru, haina

haja ya padri, mchungaji, wala wanazoita nyumba za Mungu zilizojengwa na mikono ya wanadamu. Kila mmoja wetu ana nafsini mwake patakatifu pa patakatifu, yaani Mungu.

Mazingira nayo pia inaweza kutusaidia kuepuka sala inayotamkwa akilini, wachungaji na mapadri. Tukiitunza kwa upendo inaweza badilika kuwa bustani ya Mungu inayoipa uzima hisi zetu kwa msaada wa Roho wa uhuru.

Katika kila msimu, mazingira ni ujumbe wa uumbaji, usemi wa Mungu. Katika kila msimu, mazingira hutuonyesha maua, matunda na zawadi zake. Haijisifu kwani inajua kwamba nguvu ya uumbaji inadumu kwa kuwa Mungu ni Uzima. Mwenendo wetu ungepashwa kufanana na ule wa mazingira ambao unategemea Roho muumba mwenye nguvu, au Uzima.

Neno lililo pote la Muumbaji, neno la Wamilele linasema: MIMI NDIYE YULE ALIYE-uzima wa milele.

Ukitaka, jitumbukize katika mkondo wa ulimwenguni pote wa uzima ulio ndani ya kila mmoja wetu, karibu nasi, juu na chini yetu. Ni Uzima ulio mahali pote, Mungu, Roho huru wa Baba yetu wa mbinguni ambaye sisi ni wanae.

Warithi wa Yesu wa Nazareti wanawatakia wenzi wao hata pia wao wenyewe, kukua na kukomaa kiroho katika dhamiri kwamba wawili au watatu wakikusanyika kwa jina la Kristu wa Mungu, Roho aliye hai na huru yupo kati yao, yupo kati yetu.

Ni katika dhamiri hiyo ndio ndugu na dada katika Roho huru wanawasalimu.

Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Mnaishi milele. Hakuna mauti
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Mafundisho ya Yesu Mlimani





Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mmekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake. *(Kurasa 48)*



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu. Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha.

Ila, sala halisi, huhitaji mafunzo, kwa kuwa, sala halisi, tunayoifanya ndani mwetu wenyewe, ni mazungumzo na Mungu. *(Kurasa 56)*



Amri Kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa

na kufafanuliwa katika usemi wa siku hizi, ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote. *(Kurasa 44)*

Vitabu hivi vinapatikana pia katika lugha ya kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi pia

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
Gabriele-publishing.com



Gabriele Publishing
The Word

Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany
www.gabriele-publishing.com